UKAGUZI WA MANABII WAKUBWA-Wayne Jones

Katika mfululizo wa historia ya wana wa Israeli kulikuwa na maamuzi mbalimbali na mfululizo wa matukio ambayo kwa sehemu kubwa yalibadilisha muelekeo na kuathiri maisha ya baadaye ya taifa la Israeli. Kwa mfano, Uamuzi wa Yakobo kuipeleka familia yake Misri,baada ya kutambua kwamba Yusufu bado yupo hai-mwishoni mwa kitabu cha Mwanzo, ni sababu kubwa ambayo Waisraeli waliomba ukombozi toka Misri-kama kitabu cha Kutoka kinavyoanza. Jambo jingine lililogeuza muelekeao wa historia ya Waisraeli ilikuwa ni maamuzi ya Rehoboamu-katika I Wafalme 12. Alichagua kuwasikiliza washauri vijana na kuacha kuondoa mzigo wa kodi ambao Selemani aliuweka.Badala yake,akaufanya mzito zaidi mpaka watu wakagoma na taifa kugawanyika.

Wafalme wa Kwanza 12 inathibitisha kuwa ni kipindi kikubwa cha mpito kwa Waisraeli.Kilikuwa ni kipindi cha aibu na mabishano hatimaye kiburi na mambo ya kipuuzi. Ufalme ukagawanyika na makabila 10 kati ya 12 yalikuwa chini ya utawala wa Yeroboamu ambaye aliruhusu ibada ya uongo na ukuhani wa uongo (I Wafalme 12:28-33). Kutokea hapo manabii walifanya kazi kubwa katika ufamle wa Yuda na Israeli. Ilisemekana kwamba Manabii hawa walikuwa “Watengenezaji wa Wafalme” na “Wavunjaji wa Wafalme”. Walikuwa ni Wasemaji wa Mungu ili kwamba watu waweze kusikia kile ambacho Mungu anakisema.Sio jambo la kushangaza kwamba - tunatambulishwa nabii asiyetajwa jina, ambaye anatoa ujumbe wa Mungu ambao hautasikilizwa-mwanzoni mwa I Wafalme 13. Wamekuwapo manabii katika Israeli kabla ya siku hizi, lakini sasa watakuwa ni kiini kama wazungumzaji wa Mungu kwa taifa lake. Watabaki kuwa kama vyombo maalumu cha mawasiliano kwa mataifa yaliyogawanyika, kupitia kuanguka kwa Israeli na Yuda, katika kipindi cha miaka 70 ya utumwa, na hata baada ya kurudi kwa masalia.Kwa ukengeufu wa imani zao, ujumbe wao ulikuwa ni kuwakumbusha kushindwa kwao kutii Agano lao na Mungu.Kwa ujumbe wao wenye uaminifu na uliojaa matumaini ambao waliorejea waaminifu watakumbuka utumwa wao ambao umesababisha kurudishwa katika nchi yao iliyojaa ibada za sanamu.

Baadhi ya watu hawa walijulikana kama manabii-wanenaji,kulingana na huduma yao, kama ilivyopendekezwa kulingana na cheo chao,kimsingi ilikuwa ni ujumbe wa kuzungumza.Watu kama Nathani, Eliya, na Elisha wakuwa katika kitengo hiki. walikuwepo pia manabii wa kawaida, ambao pamoja na kazi zao za kutangaza ujumbe wao, walichaguliwa na kuvuviwa kuandika unabii wao.

Manabii wakubwa wanne wanaangukia katika sehemu hii.Walikuwa ni manabii ambao waliandika zaidi ya wenzao 12 ambao walijulikana kama manabii wadogo.Kusudi la makala hii ni kupitia hao manabii wane ambapo tutaelewa vema makusudi ya huduma yao na umuhimu wa maneno waliyo yaandika.

**ISAYA**

Nabii Isaya alitabiri juu ya Yuda katika kipindi cha utawala wa Uzzia, Jotham, Ahazi, na Hezekia, ambapo anaweka maelezo yake takribani miaka 750 kabla ya kuzaliwa kwa Kristo. Kitabu cha Isaya mara kwa mara kinatambulika kama “Biblia Ndogo” Kwasababu kimejaa sura 66 zenye migawanyiko miwili. Sura ya 1-39 ikizungumzia hukumu ambayo itakuja juu ya Yuda na mataifa yanayowazunguka kwa kumkataa kwao Mungu. Isaya anaelezea namna ya unafiki walionao Yuda katika kumkaribia Mungu.Kumkaribia kwao kulikuwa ni chukizo kwa Mungu ambapo aliwaamuru kuacha kumtolea dhabihu zao hadi watakapo itakasa mioyo yao (Isaya 1:11-20). Sehemu ya Pili ya kitabu inajumla ya Sura 27 zinazosisitiza tumaini ambalo wenye haki hawana  sehemu katika mambo ya siasa, kimaadili au mambo ya kijamii dhidi ya muda wao.Kiasi cha tumaini katika sura hizi 27 ni kiwango cha tumaini linalopatikana katika ujumbe wa vitabu 27 katika Agano jipya.

Sababu ya mwisho ya tumaini la hapo juu lipo katika kiini cha ujumbe wa Isaya. Amekuwa akiitwa "Nabii wa ujumbe" kulingana na wingi wa nukuu za ujio wa Masihi. Hasa , katika uzao wa bikira (Isaya 7:14); Jina lake la ajabu (Isaya 9:6); na kukataliwa kwake, uwanadamu wake, na kusulubiwa kwake(Isaya 53) ni baadhi ya vifungu.

**YEREMIA**

Yeremia ina sauti ya mtu anayenena pamoja na moyo wa utumishi.Kwa mshangao sana, unabii wake unaanza kipindi cha kuanguka kwa madili kwa Yuda pamoja na kuanguka kwa Yerusalemu. Kama vile Yesu, Yeremia anaomboleza na kulia kwa ajili ya watu wake na ndipo anapata jina la "Nabii anayelia" kwa zaidi ya miaka 60 Yeremia amefanya kazi katika kipindi cha Wafalme watano; Yehoahazi, Yehoakimu, na Sedekia. Moja ya jambo linalozungumziwa katika uandishi wa Yeremia ni vigumu kuufuatilia mtiririko wake.Baadhi ya vipengele vimeandikwa kwa mfululizo wa vipindi, wakati vingine vipo kawaida. Hii inaweza kuwa ni ukweii kwamba maandiko yake ya kwanza yaliharibiwa (36:20) na pia nakala za maandiko ya pili zikatengenezwa. Mpangilio unaweza kuwa mgumu kwa chapisho la mara ya kwanza. Vyovyote vile,tuna maandiko yote ya Yeremia ambayo Mungu alitaka tuwe nayo. Yanabeba maonyo dhidi ya watu wakaidi, maonyo dhidi ya takribani mataifa mengine kumi kutokana na uovu wao, na mambo binafsi ambayo Yeremia anakabiliana nayo katika huduma yake(ikiwa ni pamoja na kukatishwa tamaa kiasi cha kutaka kuacha na kuumizwa katika maisha na maadui zake).

Yeremia anaandika pia kitabu cha maombolezo, ambacho ni cheusi,chenye shairi la kuomboleza juu ya kuanguka kwa Yerusalemu. Kitabu kipo katika mtindo wa fumbo lenye sura ndani yake, yapili na yanne zina jumla ya mistari 22 na kila moja ikianza na herufi ya lugha ya kiebrania. Sura ya tatu inafuatisha mtindo ule ule lakini inajumuisha mtiririko mara tatu kutokana na kuwa na mistari 66 jumla.

**EZEKIELI NA DANIELI**

Wote hawa walichukuliwa toka Israeli kwenda Babeli wakati wa siku za uhamisho na kuwatabiria watu wa Mungu wakiwa utumwani nchi ya ugenini. Ezekieli alikuwa ni mmoja wa watu Katika mto kaldea, wakati Danieli alikuwa katika sehemu hiyo. Wote walitumikia kusudi moja, lakini katika mazingira tofauti.

Jukumu la Ezekieli lilikuwa ni kutangaza juu ya ahadi za uwongo za kuishi kwa kipindi kifupi adhabu na kukazia ukweli kwamba ni uhamisho wa miaka 70 (1-24); kutangaza hukumu dhidi ya mataifa jirani kwa ajili ya kumkataa kwao Mungu (25-32); na kuwapa waliosalia matumaini ya kurudi nyumbani katika hitimisho la agizo la adhabu yao (33-48). Lakini pia kuna sauti ya kiumasihi katika unabii wa Ezekieli (tazama 33:48).

Unabii wa Danieli umegawanyika katika sehemu kuu mbili. Ya kwanza, kuna mtiririko wa matukio yanayoeleza huduma ya Danieli (1-6). Pili, maono na ndoto za Danieli zinavyo funuliwa na kutoa taarifa juu ya wakati ujao-hasa katika kipindi kati ya Maagano( 7-12). Moja ya ujumbe mkubwa katika kitabu hiki ni ule wa kuanguka na kusimama kwa falme za wanadamu, Mungu alikuwa na mpango wa ufalme udumuo milele (2:44) ambao atauanzisha wakati Mwana wa Adamu atakapoinuliwa katika siku za mwisho (7:13-14).

Ninatumaini yangu kwa mapitioi haya kwaufupi utakusaidia kuchunguza neno la Mungu. Na wote tunashukuru kazi na majukumu ya manabii na kutoa shukrani kwa Mungu ambao aliwachagua ilikutuandikia sisi.